TANGAZO LA SERIKALI Na. 58 la tarehe 26/1/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWAKATIKA ENEO LA IFUMBO YA MWAKA 2024

Jina

**1.** Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Katika Eneo la Ifumbo ya mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

**2.** Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

**3.** Mpangokina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

JEDWALI

*(Limeandaliwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba LV1 yenye majira-nukta 531076.159MS, 9034835.181KZ; baada ya hapo mpaka unelekea Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa 58º03′44″ kwa umbali wa kilomita 2.66 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba LV2 yenye majira-nukta 528814.6774MS, 9036245.69KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi kwa kufuata uelekeo wa 17º39′07″ kwa umbali wa kilomita 1.7 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba LV3 yenye majira-nukta 528299.076MS, 9037865.961KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa 62º51′11″kwa umbali wa kilomita 2.45 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba L4 yenye majira-nukta 530483.688MS, 9038985.976KZ baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa 27º36′16″ kwa umbali wa kilomita 1.85 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba LV5 yenye majira-nukta 531343.9088MS, 9040631.116KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki katika uelekeo wa 76º34′04″ kwa umbali wa kilomita 2.65 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba LV6 yenye majira-nukta 533928.8981MS, 9040013.746KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki katika uelekeo wa 12º09′00″ kwa umbali wa kilomita 2.34 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba LV7 yenye majira-nukta 534422.6939MS, 9037717.386KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa 49º15′48″ kwa umbali wa kilomita 4.41 hadi Ulipoanzia."

Dodoma,
29 Disemba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*